TUANZE

Wapatie wanafunzi wako ukarasa wa1-6 kutoka katika Kitabu cha utendakazi kwa mwanafunzi.Muipitie kwa pamoja, huku mkijibu maswali munapoendelea.

1. Maswali ya kuuliza:

a. Kwa nini unapenda kufunzwa?

b. Unawaza inaamanisha nini kuwa mfwasi wa Yesu?

c. Unatarajia kufaidia nini kutokana na mafundisho haya?

2. Amri kuu ya Mungu:

Amri kuu inapaswa kuwa ya muhimu katika vyote tunavyosema au kufanya.Wakati Yesu aliulizwa amri gani ilikuwa kuu, alijibu: “Akamwambiya, mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako na kwa akili zako zote.Hii ndio amri iliyo kuu, tena ni ya kwanza.Na ya pili yafanana nayo, nayo ni hii, mpende jirani yako kama nafsi yako.Katika amri hizi mbili hutegemea torati yote na manabi.”

(Mathayo 22:37-40, BTK)

3. Kazi kuu ya Mungu:

Amri kuu ni ya maana sana katika kutimiza kazi kuu.Kazi hii kuu inalenga wote walioamini Kristo, kwani Yesu alisema: “Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho mtakatifu; na tazama mimi nipo pamoja nanyi siku zote hata ukamilifu wa dahari.”

(Mathayo 28:19-20, BTK)

4. Maana ya Mfuasi/Mwanafunzi:

Neno ya kigiriki inayomaanisha mwanafunzi, *mathes*, haimaanishi tu “kujifunza”.Lakini ni kuungana na mwalimu wako na kuwa mfuasi wake katika yale anayoyaamini na katika tabia.

Mtume Paulo alisema, “Mnifuate mimi kama ninavyomfuata Kristo.

5. Maana ya Mkufunzi au Mwalimu (Mfanya Wafuasi):

Huyu ni mtu aliyefunzwa na kuhitimu na kuwa na silaha zote ili kuwafundisha wengine katika hali sawa na yake.

(Wakoritho 1 11:1, BTK)

Bwana Yesu alisema, “Mwanafunzi hawi mkuu kuliko mwalimu wake, lakini kila mtu ambaye amehitimu hulingana na mwalimu wake.”

(Luka 6:40, BTK)

6. Maana ya Kufanya Wafuasi:

Kufanya wafuasi ni hatua ya kujiweka wa kujiingizia (kwa mfano tabia, mwendo wa hali zako) katika watu wengine ukitarajia mavuno kutokana na kujitoa kwako.

(Luke 6:40, BTK)

UTAMBULIZI

1. Jiunganishe:

a. Fungua kwa maombi

b. Uliza maswali yafuatayo:

- Nini unapenda kufunzwa?
-Unatarajia kufaidi nini kutokana na experience hii ?

c. Changina experience yako kama mwanafunzi wa Yesu na kama mkufuzi wa Yesu.

2. Amri kuu ya Mungu:

Amri kuu inapaswa kuwa kiungo cha msingi katika vyote kunavyo sema au kufanya.Wakati Yesu alipoulizwa amri gani ndiyo iliyo kuu, akawajibu, “Akawaambia, mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote. Hii ndiyo amri iliyo kuu, tena ni ya kwanza. Na ya pili yafanana nayo, nayo ni hii: Mpende jirani yako kama nafsi yako. Katita amri hizi mbili hutegemea torati yote na manabii”.

(Mathayo 22:37-40, BTK)

3. Kazi kuu ya Mungu:

Amri kuu ya Mungu ni ya maana sana katika kutimiza Kazi Kuu. Kazi hii kuu inawalenga wakristo wote, kwani Yesu alituamuru ku

“Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu, na kuwafundusha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi, na tazama mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.”

(Mathayo 28:19-20, BTK)

4. Maana ya Mfuasi (Mwanafunzi):

Neno la kigiriki ya kumaanisha mwanafunzi, *mathetes*, haimaanishi tu “Kujifunza”, lakini ni kuungana na mwalimu wako na kuwa mfuasi wake katika yale anayoamini na katika tabia. (Neno yote jifunze katika Dictionary)

Mtume Paulo alisema: “Niigeni mimi, kama ninavyo muiga Kristo.”

(Wakorintho I 11:1, BTK)

5. Maana ya Mkufunzi au Mwalimu (Mfanya Wafuasi):

Huyu ni mtu aliyefunzwa na kuhitimu na kuwa na silaha zote ili kuwafundisha wengine katika hali sawa na yake.

Bwana Yesu alisema, “Mwanafunzi hawi mkuu kuliko mwalimu wake, lakini kila mtu ambaye amehitimu hulingana na mwalimu wake.”

(Luka 6:40, BTK)

6. Maana ya Kufanya Wafuasi:

Kufanya wafuasi ni hatua ya kujiweka wa kujiingizia (kwa mfano tabia, mwendo wa hali zako) katika watu wengine ukitarajia mavuno kutokana na kujitoa kwako.

(Luke 6:40, BTK)

Patia wanafunzi wako copy (ya Utambulizi hili) kutoka Workbook ya mwanafunzi.Muipitie kwa pamoja mkijibia maswali mnapoendelea. Ufuatilie binafsi katika juma lakufuata kwa ajili ya mazoezi na kujenga mausiano.Hatua zote 8 zinaongozwa katika wiki 8 ao 16.

UTAMBULIZI

(Kitabu cha utendakazi kwa wanafunzi)

1. Kusudi

a. Hili uwe mwanafunzi mkomavu wa Yesu kutia matendo zile Nidhamu 5 za Kiroho

b. Hili uwe mwalimu mwaminifu wa Yesu kwa kuzalisha/kuzipanua zile hatuwa 8

2. Sehemu:

a. Hatua 1 – 3 – *Ombi*

b. Hatua 4 – 8 – *Safari*

3. Kazi ya Akili

Ombi ya Kujitoa na maandiko inayolingana na *Safari*

4. Masomo ya Ziada

Ombi ya Kujitoa na ukurasa zinazolingana na *Safari*

5. Vifaa vya Mafundisho ya Biblia

Uhitimu na vifaa katika Mafunzo ya Biblia, na vile vile ya patikanayo kwenye mtandao

6. Vifaa vya Kusoma

a. Injili ya Yohana na Mtume Yohana

b. Barua kwa Warumi na Mtume Paulo

c. The Master Plan of Evangelism na Robert Coleman

7. Kazi ya ziada- Hatua 1:

a. *Nidhamu 1: Mwabudu Bwana*: Muheshimu/Msujudu – Mwongozo wa Maombi 1-6

b. *Nidhamu 2: Sikiliza Neno Lake:* Soma/Tafakari – Yohana 1-7(mlango moja kila siku)

c. *Nidhamu 3: Omba Mapenzi Yake:* Tambua/Itikia – Yohana 1-7 (mlango moja kila siku)

d.*Nidhamu 4: Ungana na Watu Wake:* Mwalimu, Washiriki wengine, Mufuasi awezekanaye

e. *Nidhamu 5: Elezea Dunia:* Changia ushuhuda wako na angalau mtu 1

f. The Master Plan of Evangelism: Mlango 1 –Soma/Tia alama

g. Ombi ya Kujitoa : Sehemu ya 1 – Tia akilini/Tafsiri/Tia katika matendo

h. Mafunzo ya Biblia ya kibinafsi: Tazama mapendekezo; chagua moja

Ombi ya Kujitoa

Mungu, Natambua kwamba nimetenda dhambi na dhambi hii inanitenga na wewe.Nakuja kwako katika toba na naamini kwambwa nimepokea msamaha wako katika Kristo.

Yesu, Naamini ulikufa msalabani kwa ajili yangu, na naungana nawe katika kufa kwa dhambi ndani mwangu. Naamini ulifufuka toka kaburini kwa ajili yangu, na naungana nawe katika ufufuko wa uzima wa milele ambao uliupana kwa neema kupitia imani.

Nakuchukua wewe Yesu, kama Mwokozi na Bwana, kukuwa nawe na kukushika kwanzia leo hata milele;

Kwa mema, kwa mabaya; kwa utajiri, kwa umasikini; katika magonjwa na katika afya;

Nikikataa wengine wote na kushikana nawe tu hata mpaka milele yote;

Nakupa maisha yangu na napokea Roho wako.

Mwongozo wa Maombi

Simameni, jueni kwamba mimi ndimi Mungu… (Zaburi 46:11)

1. Wa Umilele – Utakuwepo milele na milele

Na tangu milele hata milele ndiwe Mungu. (Zaburi 90:2)

2. Muumbaji – Uliumbwa bila chochote

Hapo mwanzo Mungu aliumba Mbingu na nchi. (Mwanzo 1:1)

3. Mwenye uweza-Unatawala juu ya uumbaji wote

Mwenye uweza peke yake, mfalme wa wafalme, Bwana wa mabwana. (Timoteo1 6:15)

4. Bwana – Unaongoza uumbaji wote

Bwana aliweka kiti chake cha enzi mbinguni, na ufalme wake unavitawala vitu vyote. (Zaburi 103:19)

5. Mtakatifu – Wewe ni Mkalifu

Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, ni Bwana wa majeshi; dunia yote imejaa utufufu wake. (Isaya 6:3)

6. Mungu – Uko peke yako

Mimi ni wa kwanza, na mimi ni wa mwisho; zaidi yangu mimi hapana Mungu. (Isaya 44:6)

7. Mwenye nguvu – Unaweza fanya chochote wakati wowote

Yasiyo wezekana kwa mwanadamu yawezekana kwa Mungu. (Luka 18:27)

8. Upo pahali pote – Unapatikana pahali pote kwa wakati moja

Kama ningepanda mbinguni, wewe uko; ningefanya Kuzimu Kitanda changu, wewe uko. (Zaburi 139:8)

9. Unajua vyote: Unaelewa vitu vyote na watu wote

Jinsi zilivyo kuu utajiri na hekima na maarifa ya Mungu, hukumu zake hazichunguziki, wala njia zake hazitafutikani. (Warumi 11:33)

10. Mwenye upendo: Unapenda pasipo kujali hali na bila mwisho

Kwa maana ginsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwana wake wa peke. (Yohana 3:16)

11. Natambua Ukuu wako

Bwana ndiye mkuu mwenye kusifiwa sana, wala ukuu wake hautambulikane. (Zaburi 145:3)

12. Nashukuru Uzuri wako

Mshukuruni Bwana kwa kuwa ni mwema, fadhili zake ni la milele. (Zaburi 136:1)

13. Baba Milele – Unalinda na Kuhangaikia/Kutusaidia

Mungu kwetu sisi ni kimbilio na nguvu, msaada utakaoonekana tele wakati wa mateso. (Zaburi 46:1)

Na Mungu atawajazeni kila mnachokihitaji kwa kadiri ya utajiri wake, katika utukufu, ndani ya Kristo Yesu. (Wafilipi 4:19)

14. Ndugu Milele – Ukomboa na kurejesha

Katika yeye huyo, kwa damu yake; tunao ukombozi wetu, msamaha wa dhambi, sawa sawa na wingi wa neema yake. (Waefeso 1:7)

Mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepite tazama! Yamekuwa mapya. (Wakorintho 2 5:17)

15. Mpenzi milele – Unafariji na kuhukumu

Nami nita mwomba Baba, naye atawapa msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele. (Yohana 16:8)

16. Nioshe

Unioshe kabisa na uovu wangu, unitakase dhambi zangu. (Zaburi 51:2)

17. Nijaze

Tena msilewe kwa mvinyo, ambamo mna ufisadi; bali mjazwe Roho. (Waefeso 5:18)

18. Niongoze

Neno lako ni taa ya miguu yangu na mwangaza kwa njia yangu. (Zaburi 51:2)

- Maandiko yaliyonukuliwa yametoka katika Tafsiri ya Biblia Takatifu (BTK)

NIDHAMU 5 ZA KIROHO



Za juu 5	**Nidhamu za Kiroho**	**Mistari ambatanishi**
Nidhamu # 1	**Mwabudu Bwana**	**Yohana 4 :24**
« Mungu ni Roho, nao wamwabuduo imewapasa kumwabudu katika roho na kweli. »		
Nidhamu # 2	**Sikiliza Neno Lake**	**Yohana 8 :31**
« Ninyi mkikaa katika neno langu, mmekuwa wanafunzi wangu kweli kweli. »		
Nidhamu # 3	**Omba Mapenzi Yake**	**Yohana14 :13**
« Nanyi mkiomba neno lolote kwa jina langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana. »		
Nidhamu # 4	**Ungana na Watu Wake**	**Yohana15 :12**
« Amri yangu ndio hii, mpendane, kama nilivyowapenda ninyi. »		
Discipline # 5	**Elezea Dunia**	**Yohana 20 :21**
« Amani iwe kwenu; kama Baba alivyonituma mimi, mimi nami nawapeleka ninyi. »		

❖ Maandiko yaliyo nukuliwa yametoka katika tafsiri ya Biblia Takatifu (BTK)

SAFARI

Safari ni chombo cha uingilisti ambayo itakusaidia kushuhudia imani yako na wengine kwa urahisi. Inaonyesha ginsi gani Kristo alilipa dharama ya dhambi na kuurejesha au kurekebisha uhuusiano wetu na Mungu ambao ulikuwa umevunjika. Kuna sehemu tano ya *Safari*, na kila mmoja inasindikizwa na andiko na mfano wakuufanana. Maneno yafuatayo yanaeleza maana ya *Safari*:

1) *Tatizo* katika maisha ni dhambi, kwamaana wote ni wakosefu.
2) *Hukumu* inayotokana na shida hii au kosa hili ni kifo.
3) *Malipo* ya dhambi inatokana kupitia kifo cha Yesu.
4) *Hatua* inahitajika kupokea malipo haya ni kupitia imani.
5) *Kusudi* ambalo inafuata imani ni upendo wa Mungu kwa watu.

Maandiko amabayo yanaunga mkono *Safari* yanatoka katika barua ya Paulo kwa Warumi.Mifano ya kuambatana yanarahisisha kuelewa *Safari* unapoiongea kwa watu wengine.



Maneno	**Mistari ya kutia Akili**	**Mifano**
***Tatizo* ni DHAMBI**	**Warumi 3 :23**	**Darts/Dartboard**
« Kwa maana wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu na Mungu. »		
***Hukumu* ni KIFO**	**Warumi 6 :23**	**Msahara/Talanta**
« Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti, bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo yesu Bwana wetu. »		
***Malipo* ni KRISTO**	**Warumi 8 :3**	**Hukumu/Haki**
« Maana yale yasiyo wezekana kwa sheria, kwa vile ilivyokuwa dhaifu kwa sababu ya mwili, Mungu kwa kumtuma mwanawe mwenyewe katika mfano wa mwili wa dhambi, alihukumu dhambi katika mwili. »		
***Hatua* ni IMANI**	**Warumi 10 :9**	**Check/Cash**
« Ukikiri katika kinywa chako kwamba yesu ni bwana, na kuamini katika moyo wako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. »		
***Kusudi* ni UPENDO**	**Warumi 13 :10**	**Tia hazina/Rudisha**
« Pendo halimfanyi jirani neno baya; basi pendo ndio utimilifu wa sheria. »		

❖ Maandiko yaliyo nukuliwa yametoka katika tafsiri ya Biblia Takatifu (BTK)

MIFANO KATIKA SAFARI

1. <u>Darts/Dartboard</u> inaonyesha *Shida* ambayo ni DHAMBI:

Mungu ni Upendo na Kutokana na Upendo alikuumba ukapate kufurahia uhusiano wa kibinafsi pamoja naye milele, lakini upendo wa kweli inapashwa kuwa wazi kuchagua ya Mungu au nafsi. Kwa bahati mbaya tulichagua kufurahisha nafsi mbele ya Mungu, na pale tukaleta shida ya utengano.Waziya mchezo darts ambayo inasheria ya kwamba unahitajika kudona katikati wakati wote ili yakwamba ukapate kushinda. Ukidona katikati mara nne juu ya mara tano na mimi nidone mara moja juu ya tano, nani ameshinda? Hakuna aliye shinda, kwa sababu sheria inasema kudona katikati kila mara. Kiwango cha Mungu ni ukamilifu; kwa hivyo, dhambi moja inatosha kututenga na Mungu.

2. <u>Mshahara/Zawadi</u> inaonyesha *Hukumu/Ghadabu*, ambayo ni KIFO:

Kama una kibarua/kazi unapokea mshahara kwa sababu ya kazi uliyoifanya.Zawadi haiko kitu unachopokea kwa sababu unastahili, lakini ni kitu ambacho unapokea kutokana na gharama ya mwengine mtu. Tumepokea mshahara wa kifo kwa kutokana na kazi zetu ambazo kulimfanyia Mungu, lakini amechagua kutupatia zawadi ya uzima wa milele kwa gharama ya mwana wake, Yesu Kristo.

3. <u>Hukumu/Haki</u> inaonyesha *Malipo*, ambayo ni KRISTO:

Unakamatwa kwa kosa ambalo ina hukumu ya kifo.Unapofika kotini, hakimu anakwambia uanze kujitetea. Na kwa sababu unajua kuna ushaidi wa kutosha kuusu makosa yako unaitika makosa yako. Na hakimu naye anaitikia na kusema unahukumiwa kulingana na makosa yako. Na pale unajihisi kama hauna tena tumaini, kwa ghafla hakimu anasema « kungali tumaini kwa ajili yako. » Na pale hakimu ananyanguka na kuja pembeni yako na anasema, « Nitalipa gharama kwa ajili yako na maisha yangu ili yakwamba ukapate haki, na ukapate kuwa huru. » Mungu ni hakimu aliyekuja duniani kwa mwili kama Yesu ili akalipe gharama kwa dhambi zetu na maisha Yake kwa kukufa msalabani kwa niaba yetu.

4. <u>Check/Cash</u> inaonyesha *Hatua*, ambayo ni IMANI:

Ukiitika malipo kutoka kwa mtu fulani kwa njia ya check, pale unaonyesha imani kwa mtu yule kuwa na fedha/pesa katika accounti yake kwenye benki. Na vile vile check haina kazi mpaka pale utakapo chukua hatua ya imani na kwenda kwenye benki ili yakwamba wakapate kugeuza ile check iwe cash. Na vile vile, imani kwa Mungu sio tu kujuwa kuusu zawadi yake ya uwokovu, lakini kwa kuitendea kazi kwa kumwamini Kristo na yale ambayo anapana ambayo ni uzima wa milele.

5. <u>Wekesha/Rudisha</u> inaonyesha *Kusudi* ambayo ni UPENDO:

Unapowekesha pesa kwenye kampuni fulani unatarajia malipo au zirudie. Na hilo ndio kusudi la kila muwekezagi. Mungu anapowekesha upendo wake kwako kupitia Mwana wake na nguvu za roho wake, Anatarajia kurudishwa. Matarajia ya kurudisha ambayo Mungu anataka ni upendo. Kusudi la Mungu ni kuzalisha au kuzidisha upendo wake kwetu na kupitia ndani yetu. Na kusudi letu ni kumuacha.

Safari mbali na Mungu/isiyoelekea kwa Mungu inatokana na dhambi zako.

Safari inayoelekea kwa Mungu inatokana na imani yako kwa Kristo.

HATUA YA 1

1. Fungua kwa Maombi

2. Ushuhuda "Historia yako" / "Historia yake"

a. Changia « Hadithi yako (ushuhuda) na wanafunzi wako.

b. Karibisha wanafunzi wako kuchangia ushuhuda zao vile vile.

c. Wazia kwa maakini sehemu ya 1 ya *Ombi ya kujitoa* –"Historia Yako"

d. Wazia kwa maakini sehemu ya 2 ya *Ombi ya kujitoa* – "Historia Yake"

3. Tazama nidhamu za kiroho – Uliza maswali yafuatayo:

a. *Nidhamu 1:* Ni ginsi gani Mwongozo wa Maombi umekusaidia kumwabudu Bwana?

b.*Nidhamu 2:* Mungu alikuzungumia nini baada ya kusoma Yohana 1-7?

c.*Nidhamu 3:* Mungu alikuongoza kuombea nini baada ya kusoma Yohana 1-7?

d. *Nidhamu 4:* Ulifanya ushirika na nani, na muliendelea namna gani?

e.*Nidhamu 5:* Ulichangia injili na nani na muliendelea namna gani?

4. The Master Plan of Evangelism – Tia alama kwanzia Mlango wa 1

5. Vifaa vya Mafunzo ya Biblia:

a. Eleza dhamani ya mafundisho ya Biblia; onyesha kile unacho tumikisha na useme sababu gani.

b. Kama mafundisho inahitajika, saidia wanafunzi kwa vile ambavyo vinahitajika.

6. Kujukumika /Maombi:

a. Ongea kuusu kujukumika, na dhamani ya kukuwa katika uhusiano wa aina hiyo.

Soma mstari huu na muijadili matumizi yake kulingana na kujikumika:

« Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuompeana, mpate kuponywa, kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana, ukiomba kwa bidii. »

(Yakobo 5:16, BTK)

b. Onyesha mfano kwa kuchangia jambo ambalo linahitaji kuchukuliwa.

c. Karibisha wanafunzi wako wafanye vile vile, bila kufanya wasikie wanalazimishwa.

d. Muombeane mumoja kwa mwingine mukilenga maneno la kujumika.

7. Mafundisha ya Biblia

a. Taja umuhimu wa kutafsiri neno la Mungu kwa usawa.

Soma huu mstari na ujadili matumizi kulingana na Mafunzo ya Biblia:

« Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli. »

(Tim 2 2:15, BTK)

b. Eleza ginsi ya kujifunza ukitilia mkazo mambo matatu:

1. Mtazamo: - Ona picture kubwa kwa kusoma maandiko (kwa mfano sehemu ya 1 ya Ombi ya kujitoa) katika yaliomo (kwa mfano sehemu zote 3 ya Ombi ya kujitoa).

2. Utafsiri**:** Tafuta makusudi ya mwandishi na utafute maneno msingi ili ukapate kuelewa maana ya text, kwa kutumia akili zako.

3. Kutia katika matendo: Katika mwanga wa utafsiri, tia text katika matendo kibinafsi.

8. Mafundisho ya maneno- Sehemu ya 1 ya *Ombi:*

Wote waseme Sehemu ya 1; ambia wanafunzi watoe maana kutoka katika kamusi ya maneno msingi.

Mungu, natambua kama nimetenda dhambi, na kwamba dhambi zangu zimenitenga nawe.Nakuja kwako katika toba na napokea msamaha wako katika Kristo.

Mfano:

Natambua - kuelewa vizuri na kwa usawa

Dhambi - kosa dhidi ya dini au tabia njema, kwenda kinyume na sheria ya Mungu

Kutenga -kutoa kitu katika sahemu yake, mbali na zingine

Toba-kijihisi mwenye kujihukumu, kubadilisha mawazo, kugeuka mbali na dhambi

Kupokea -kuchukua, kumiliki

Msamaha -tendo la kusamehe kosa

Kristo-Messiah, kujitambulisha kwa Mungu katika njia takatifu

9. Utafsiri-Sehemu ya 1 ya *Ombi:*

Acha wanafunzi wako watafsiri Sehemu ya 1 ya *Ombi* kwa akili zao.

Mfano:

Katika hili ombi la kibinafsi kwa Mungu ni vitu 3 vinahitajika hili uhusiano nae ukapate kurudishwa.Yule ambaye hatii anapaswa tambua makosa yake kwa Mungu na ginsi gani makosa yake imemtenga na Mungu.Cha pili hukumu yakutoka moyoni inapaswa pokea msamaha wa Mungu ambao umetolewa katika Kristo.

10. Kutia Katika matendo-Sehemu ya 1 ya *Ombi:*

Acha wanafunzi wako waitie katika matendo Sehemu ya 1 ya *Ombi* kulingana na utafsiri.

Mfano:

Kutengeneza wakati wote ninapotenda dhambi ili nikapate kukaa karibu katika uhusiano wangu na Mungu.

11. Funga kwa Maombi:

a. Eleza umuhimu wa kuomba mapenzi ya Mungu na ginsi gani maombi ya uaminifu inapaswa fatwa na matendo ya kujukumika, ginsi inayoonekana katika huu mstari:

"Muwe wenye kulishika Neno, wala si wenye kusikiliza tu, mkijidanganya wenyewe."

(Yakobo1:22)

b. Acha wanafunzi wako waombe na ma application zao katika akili.

10. Kazi ya ziada – Hatua 2:

a. *Nidhamu 1: Mwabudu Bwana:* Muheshimu/Msujudu – Mwongozo wa Maombi 1-12

b. *Nidhamu 2: Sikiliza Neno Lake:* Soma/Tafakari – Yohana 8-14 (mlango moja kila siku)

c. *Nidhamu 3: Omba Mapenzi Yake:* Tambua/Itikia – Yohana 8-14 (mlango moja kila siku)

d.*Nidhamu 4: Ungana na Watu Wake:* Mkufunzi; Wafuasi Wenzako, Mwanafunzi anayestahili.

e. *Nidhamu 5: Elezea Dunia:* Changia ushuhuda wako na angalau watu 2.

f. The Master Plan of Evangelism: Mlango wa 2 – Soma na Tia alama

g. Ombi ya kujitoa: Sehemu ya 2/Tia akilini/Tafsri/Tia katika matendo

h. Jifunze Biblia : Kuwa na uzoefu na utangulizi wa Kitabu.

HATUA YA 2

1. Fungua kwa Maombi

2. Pitia tena Nidhamu za kiroho – Uliza maswali yafuatayo:

a.*Nidhamu 1:* Ni ginsi gani ule mwongozo wa kiroho ulikusaidia kumwabudu Bwana?

b.*Nidhamu 2: Mungu* alikuzungumzia nini ulipokuwa nasoma Yohana 8-14?

c.*Nidhamu 3: Mungu* alikuongoza kuombea nini ulipokuwa nasoma Yohana 8-14?

d.*Nidhamu 4:* Ulifanya ushirika na nani? Na iliendelea je?

e.*Nidhamu 5:* Ulichangia injili na nani? Na iliendelea je?

3. The Master Plan of Evangelism –Uliyoyachagua kutoka Mlango 2

4. Jifunze Biblia – Jadili yaliomo

5. Kujukumika/Maombi

a. Changia maswala binafsi ya kujukumika katika ujasiri.

b. Ombeaneni mmoja kwa mwingine kuusu maswala ya kujukumika.

6. Mafundisho ya Neno – Sehemu ya 2 ya *Ombi*:

Acha wanafunzi wako watoe maana katika kamusi ya maneno msingi .

Yesu, Naamini ulikufa msalabani kwa ajili yangu na naungana nawe katika kifo kwa dhambi. Naamini yakwamba ulifufuka toka wafu kwa ajili yangu, na naungana nawe katika ufufuko kwa uzima wa milele, ambao uliipana kwa neema kupitia imani.

7. Utafsiri – Sehemu ya 2 ya *Ombi*

Acha wanafunzi watumie sehemu ya 2 ya *Ombi* kulingana na utafsiri.

Mfano:

Zawadi ambayo tuliipokea katika Sehemu ya 1 inazungumziwa katika Sehemu ya 2 . Injili ni ya kibinafsi. Yesu alikufa kwa ajili ya dhambi zangu, na sasa naufisha mwili wangu kwa njia za dhambi.

Yesu alipata ushindi kwa kifo, na nafufuka naye katika uzima wa milele, ambao aliupana kama zawadi kwa wale wote waliotia tumaini lao kwake.

8. Matumizi – Sehemu ya 2 ya *Ombi*

Acha wanafunzi watafsiri Sehemu ya 2 ya *Ombi* kwa akili yao.

Mfano:

Kutia imani yangu katika matendo kwa kukufa kwa dhambi na kuuishi kwa ajili Yake tu.

9. Funga kwa Maombi

10. Kazi ya ziada – Hatua 3:

a. *Nidhamu 1: Mwabudu Bwana:* Muheshimu/Msujudu – Mwongozo wa Maombi 1-18

b. *Nidhamu 2: Sikiliza Neno Lake:* Soma/Tafakari – Yohana 15-21 (mlango moja kila siku)

c. *Nidhamu 3: Omba Mapenzi Yake:* Tambua/itikia – Yohana 15-21 (mlango moja kila siku)

d.*Nidhamu 4: Ungana na Watu Wake:* Mkufunzi; Wafuasi Wenzako, Mwanafunzi anayestahili

e. *Nidhamu 5: Elezea Dunia:* Changia ushuhuda wako na angalau watu 3

f. The Master Plan of Evangelism: Mlango wa 3 – Soma na Tia alama

g. Ombi ya kujitoa: Sehemu ya 3/Tia akilini/Tafsri/Tia katika matendo

h. Jifunze Biblia : Kuwa na uzoefu na Utangulizi wa Vitabu.

HATUA YA 3

1. Fungua kwa Maombi

2. Pitia tena Nidhamu za kiroho – Uliza maswali yafuatayo:

a.*Nidhamu 1:* Ni ginsi gani ule mwongozo wa kiroho umekusaidia kumwabudu Bwana?
b.*Nidhamu 2: Mungu* alikuzungumzia nini ulipokuwa nasoma Yohana 15-21?
c.*Nidhamu 3: Mungu* alikuongoza kuombea nini ulipokuwa nasoma Yohana 15-21?
d.*Nidhamu 4:* Ulifanya ushirika na nani? Na iliendelea namna gani?
e.*Nidhamu 5:* Ulichangia ingili na nani? Na iliendelea namna gani?

3. The Master Plan of Evangelism – Uliyoyachagua kutoka Mlango 3

4. Jifunze Biblia – Jadili Utangulizi wa Vitabu

5. Kujukumika/ Maombi :

a. Changia maswala binafsi ya kujukumika katika ujasiri.
b. Ombeaneni mmoja kwa mwingine kuusu maswala ya kujukumika.

6. Mafunzo ya Neno – Sehemu ya 3 ya *Ombi:*

Wote waseme Sehemu ya 3; acha wanafunzi watoe maana ya maneno msingi kutokana katika kamusi.

Nakuchukuwa wewe, Yesu, Kama Mwokozi na Bwana, kukuwa nawe na kukushika kuanzia leo na kuendelea; kwa vizuzi na kwa mabaya; katika utajiri, na katika umasikini, katika magonjwa na katika afya; nakataa wengine wote na kushikana na wewe tu katika umilele yote.Nakupatia maisha yangu, na napokea Roho Wako.

7. Utafsiri – Sehemu ya 3 ya *Ombi* :

Acha wanafunzi watie katika matendo Sehemu ya 3 ya *Ombi* kulingana na utafsiri.

Mfano :

Sehemu ya 3 inaonyesha kujitoa kikamilifu kwa Yesu. Ni kama vile agano la ndoa, ambao inaoresha upendo halisi, unavunja mausiano yasio ya Kimungu, na unahakikisha kujitoa na kuvumilia katika Yesu milele. Wakati waamini wanajitoa katika hali hii, Bwana hujibu kwa kuwapatia Roho Mtakatifu.

8. Kutia katika matendo – Sehemu ya 3 ya *Ombi:*

Acha wanafunzi wako watafsiri Sehemu ya 3 ya *Ombi* kwakutumia akili zao.

Mfano:

Kusimamisha imani kila siku kwa siku kwa kurudilia lile agano kwa Yesu Kristo.

9. Funga kwa Maombi

10. Kazi ya ziada – Hatua 4:

a.*Nidhamu 1: Mwabudu Bwana:* Tazama Ukuu na Uziri wa Mungu
b.*Nidhamu 2: Sikiliza Neno Lake:* Soma Warumi1-3/ Tia akilini Warumi 3:23
c.*Nidhamu 3: Omba Mapenzi Yake:* Mwitikie Mungu unaposoma Warumi 3:21-23
d.*Nidhamu 4: Ungana na Watu Wake:* Jiunge katika kufanya wafuasi na ushirika
e.*Nidhamu 4: Elezea Dunia:* Changia ushuhuda wako na angalau watu 3
f. The master Plan of Evangelism: Mstari wa 4 – Soma na Utie alama
g. Mafunzo ya Biblia: Kuwa na uzoefu na Vinavyolingana.

HATUA YA 4

Tatizo

Mungu ***Sisi***

Upendo **<u>Dhambi</u>**

1. Fungua kwa Maombi
2. Kiri lile *Ombi* na *Safari* – Warumi 3:23
3. Nidhamu za Kiroho – Uliza Maswali yafuatayo:
a.*Nidhamu 1:* Ni ginsi gani wakati wako wa maabudu umegusha maisha yako?
b.*Nidhamu 2: Mungu* alinena nawe nini ulipokuwa ulisoma Warumi 1-3?
c. *Nidhamu 3: Mungu* alikuongoza kuombea nini ulipokuwa nasoma lile Andiko?
d.*Nidhamu 4:* Ulifanya ushirika na nani? Na iliendelea je ?
e.*Nidhamu 5:* Ulihubiri na nani, na iliendelea vipi ?
4. The Master Plan of Evangelism – vitu uliuvyoona katika Mlango wa 4
5. Jifunze Biblia-Tia katika matendo ukitumia Viambano (Concordance)
6. Changia /Abudu/Omba
a.*Changia* – Maneno/Maswala binafsi na kujukumika katika ujasiri
b.*Abudu* – Tambua Ukuu wa Mungu /Shukuru Uzuri wa Mungu
c.*Omba* – maswala ya kujukumika/Mtazamo katika Neno la Mungu: Warumi 3:21-23
7. Mtazamo –Warumi 3:21-23:
a. Wote warudilie: *Ombi ya Kujitoa* na Warumi 3:23
b. Acha wanafunzi wapane Mistari ya Mtazamo ili wapate *kuhisi ile sura kubwa (mtazamo kubwa).*
Mfano:
Biblia inafundisha ya kwamba haki haikuji kwa kushika sheria za Mungu, lakini tu kwa kupitia katika njia ya imani kwa Yesu kristo kwa sababu kila mtu ana dhambi.

8. Utafsiri – Warumi 3:21-23
a. Ambia wanafunzi wasome kila mstari (mifano yalio chini yametoka katika BTK).
b. Ambia wanafunzi watoe maana kutoka kwenye kamusi ya Maneno Msingi katika kila mlango.
c. Ambia wanafunzi watafsiri kila mlango kwa maneno yao & vifaa vya mafunzo.
d. Raisisha ujadiliano kuusu maana ya kila mlango katika yaliomo.

3:21 Lakini sasa haki ya Mungu imedhihirishwa pasipo sheria: Inashuhudiwa na torati na manabii-

Haki - Kufikia kiwango cha kile ambacho kiko sawa (vile vile 3:22)
Imedhihirishwa: Kuonekana waziwazi katika macho au ufahamu
Sheria - Sehemu ya kwanza ya ugawanyo ya maandiko ya Wayahudi; Vitabu 5 vya Musa.
Manabii - Sehemu ya pili ya ugawanyo ya maandiko ya Wayahudi
Inashuhudiwa - Kusema yale ambayo mtu ameyaona na kuyasikia

Uhusiano ulio sawa na Mungu hauji kupitia uwezo wa mtu wa kushika sheria za Mungu, kwa sababu hukuna anayeweza kuufikia utimilifu wake (Warumi 3:10-20). Hii kweli inaungwa mkono na kila kitu kilichoandikwa katika Agano la Kale.

3:22 Ni haki ya Mungu iliyo kwa njia ya imani katika Yesu Kristo kwa wote waaminio. Maana hakuna tofauti.
Imani - Hali kuwa na uhakika katika kitu fulani/au mtu, bila kujali hali
Kristo - Messiah, ginsi ilivyoelezwa na manabii wa maandiko ya Waebrania
Waaminio - Kuwa na msimamo mkuu, kuitika kama ukweli
Tofauti - Ubaguzi inayofanyika kati ya vitu visivyo sawa

Uhusiano ulio sawa na Mungu hunatokana na kumwamini Messiah. Wale wote wanawo mwamini Yesu wanafanywa wenye haki na Mungu, wote Wayahudi na Wayunani (Warumi 3:29). Mungu habagui/kutafutisha kati ya Myahudi wala asiye Myahudi.

3:23 Kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu.

Wamefanya dhambi - ni kitendo cha kuvunja kanuni za dini
Utukufu -heshima kuu; uzuri mkuu.

Watu wote wana kosa la kuvunja kanuni/sheria za Mungu (Warumi 3:9).Kila mtu anakosa alama ambazo Mungu anahitaji katika maisha yetu.Ambayo ni kuwa sawa naye katika uzuri wa utukufu.

8. Kutia katika Matendo – Warumi 3:21-23:
Kutambua dhambi ni tatizo la dunia yote ambayo inashindwa tu na kazi ya ukombozi iliyofanywa pale msalabani (neno la msingi la kukumbuka ni dhambi.)
9. Funga kwa Maombi
10. Kazi ya ziada-Hatua 5:
a. *Nidhamu 1: Mwabudu Bwana:* Tazama Ukuu wa Mungu na Uzuri Wake
b. *Nidhamu 2: Sikiliza Neno Lake:* Warumi 4-6/Tia akilini Warumi 6:23
c. *Nidhamu 3: Omba Mapenzi Yake:* Mwitikie Mungu unaposoma Warumi 4-6
d. *Nidhamu 4: Ungana na Watu Wake:* Jihusishe Katika Ushirika na Kufanya wafuasi
e. *Nidhamu 5: Elezea Dunia :* Changia *Omb*i na angalau watu 3
f. The Master Plan of Evangelism: Mlango wa 5 -Soma na Tia alama
g. Soma Biblia: Kuwa na uzoefu na mifano ya hapa na pale (Cross References).

HATUA YA 5

Hukumu

Mungu | | ***Sisi***

Dhambi

Kifo

1. Fungua kwa Maombi
2. Rudilia lile *Ombi* na *Safari* – Warumi 3:23, 6:23
3. Nidhamu za Kiroho – Uliza Maswali yafuatayo:
a. *Nidhamu 1:* Ni ginsi gani wakati wako wa muabudu uliongoza maisha yako?
b. *Nidhamu 2:* Mungu alinena nawe nini ulipokuwa ulisoma Warumi 4-6?
c. *Nidhamu 3:* Mungu alikuongoza kuombea nini ulipokuwa na soma Andiko?
d. *Nidhamu 4:* Ulifanya ushirika na nani? Je iliendelea namna gani ?
e. *Nidhamu 5:* Ulicyangiya Neno na nani ? Na iliendelea vipi ?
4. The Master Plan of Evangelism – vitu uliuvyoona katika Mlango wa 5
5. Vifaa vya Mafunzo ya Biblia -Tia katika Matendo ukitumia vifanananishi (Cross References)
6. Changia /Abudu/Omba
a. *Changia*: - Maswala binafsi ya kujukumika katika ujasiri
b. *Abudu* – Tambua Ukuu wa Mungu /Shukuru Uzuri wa Mungu
c. *Omba* – Maswala ya kuchukuliana/Mtazamo katika Neno la Mungu: Warumi 6:21-23
7. Mtazamo –Warumi 6:21-23:
a. Soma Warumi 6:21-23 katika matafsiri mawiili ukapate *kuona mtazamo kubwa.*
b. Ambia wanafunzi watoe Mstari wa Mtazamo ili wakapate *kuhisi mtazamo kubwa.*
Mfano:
Watu hawawezi kuwa wenye haki kwa kushika Sheria na yale Manabii wanayo sema, lakini kwa Kumwamini Yesu. Dhambi za mwanadamu zinahukumu, lakini neema ya Mungu inakomboa.

8. Utafsiri – Warumi 6:21-23
a. Ambia wanafunzi wasome kila mstari (mfano ulio chini ulitoka katika BTK).
b. Ambia wanafunzi watoe mfano ya Maneno Msingi kutoka katika kila mstari.
c. Ambia wanafunzi watafsiri kila mstari kutumia akili zao & vyombo vya kusoma.
d. Ingilia katika kujadili kila mstari na kutoa maana yake katika context.

6:21 Ni faida gani basi mliyopata siku zile kwa mambo hayo mnayoyataharikia sasa? Kwa maana mwisho wa mambo haya ni mauti.

Faida- msahara unatokana na matendo au kazi (vile 6:22)
Kutahayarika – kusikia kuwa haufahi, haustahili au mwenye kosa
Mauti - mwisho wa maisha, kukosa maisha ya kiroho (vile 6:23)

Kama tabia mbaya hazikuwasaidia wakristo kabla hawaamini kwani zilileta aibu na kifo, zile tabia hazitawasaidia hata baada ya kuokoka.

6:22 Lakini sasa mkiisha kuwekwa huru, na kuwa mbali na dhambi na kufanywa watumwa wa Mungu, mnayo faida yenu, ndiyo kutakaswa, na mwisho wake ni uzima wa milele.

Huru - Kutokuwa chini ya uongozi au utawala wa mtu yeyote ule
Dhambi - Kutotii au kugeuka sheria za kiroho/Mungu (vile 6:23)
Watumwa - Kuwa chini ya mamlaka ya mtu fulani (kuwa kifungoni)
Umilele - Isiyokuwa na mwisho (vile 6:23)
Uzima - Uwepo wa kiroho unaozidi uliyo baada ya kifo cha mwili wa kawaida (vile 6:23)

Wakati Mungu anakomboa wanadamu kutoka tabia mbaya anawafanya Wake. (Angalia Warumi 6:17-18) .Wale wanao tawaliwa na Mungu hupokea baraka za utakatifu na uzima wa milele mbinguni.

6:23 Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti, bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu .

Mshahara- Malipo kwa kazi au huduma iliyotolewa
Karama- Kitu kinachopanwa bure bila malipo yoyote
Bwana: Mtu mwenye nguvu na mamlaka (mfano Mungu; Yesu)

Malipo ya dhambi ni kifo (Kutengwa na Mungu milele), lakini zawadi (Karama) ya Mungu ni uzima (mfano: uhusiano na Mungu milele).Hii zawadi ni kwa wale tu ambao wanamwacha Yesu aongoze maisha yao, ambao ndio maana ya yeye kuwa Bwana wetu.

9. Kutia katika Matendo - Warumi: 6:21-23

Kuona kifo kama ghadhabu na uzima kama zawadi ya Mungu, na kushukuru kwamba kifo sio tena makao yangu ya milele (neno la msingi ya kukumbuka ni kifo.)

10. Funga kwa Maombi

11. Kazi ya ziada– Hatua 6:

a. *Nidhamu 1: Mwabudu Bwana:* Angalia Ukuu na Uzuri wa Mungu
b. *Nidhamu 2: Sikiliza Neno Lake:* Soma Warumi 7-9/Tia akilini Warumi 8:3
c. *Nidhamu 3: Omba Mapenzi Yake:* Mwitikie Mungu unaposama Warumi 7-9
d. *Nidhamu 4: Ungana na Watu Wake:* Jiunge katika ushirika na kufanya wafuasi
e. *Nidhamu 5: Elezea Dunia* : Changia Ombi na angalau watu 3
f. The Master Plan of Evangelism: Mlango wa 6- Soma na Tia alama
g.Jifunze Biblia : Kuwa na uzoefu na ramani (maps) za Biblia.

HATUA YA 6

Malipo

Kristo



1. Fungua kwa Maombi

2. Rudilia *Omb*i na *Safari* ,Warumi 3 :23, 6 :23, 8 :3

3. Nidhamu za Kiroho – Uliza maswali yafuatayo :

a. *Nidhamu 1 :* Ni ginsi gani wakati wako wa muabudu umeaongoza maisha yako?

b.*Nidhamu 2:* Mungu alikunenea nini ulipokuwa unasoma Warumi 7-9 ?

c.*Nidhamu 3:* Mungu alikuongoza kuombea nini ulipokuwa na soma Andiko?

d. *Nidhamu 4:* Ulifanya ushirika na nani? Je iliendelea namna gani ?

e. *Nidhamu 5:* Ulicyangiya neno na nani, na iliendelea vipi ?

4. The Master Plan of Evangelism – Ulivyochagua kutoka katika Mlango wa 7

5. **Vifaa vya Mafunzo ya Biblia –Tumikasha ma Maps kutoka katika Biblia**

6. Changia /Abudu/Omba:

a. *Changia:* - Maswala ya kibinafsi katika ujasiri

b. *Abudu:* – Tambua Ukuu wa Mungu /Shukuru Uzuri wa Mungu

c.*Omba:* – Maswala ya kujukumika/Tazamo katika Neno la Mungu: Warumi 8:1-3

7. Mtazamo –Warumi 8:1-3:

a. Soma Warumi 8:1-3 kutoka katika matafsiri mawili kwa *kutazama mtazamo kubwa*.

b. Ambia wanafunzi wafanye mtazamo kwa *kuhisi mtazamo kubwa*.

Mfano:

Hakuna hukumu katika Kristo, kwa sababu alifanya yale ambayo sheria haingeifanya kwa kuweka walioamini huru, kutokana na dhambi na kifo kupitia kifo chake.

8. Utafsiri – Warumi 8:1-3:

a. Acha wanafunzi wasome kila mstari (mifano zilizo chini zimetoka katika BTK).

b. Acha wanafunzi wapane maana ya Maneno Msingi katika kila mstari.

c. Acha wanafunzi watafsiri kila mstari kutumia akili zao.

d. Waambia wajadili maana ya kila mstari katika context.

8:1 Sasa, basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu.
Hukumu: - Neno la Kuhukumu. (vile 8:3)
Kristo: - Utambilisho, mfano mkuu wa Mungu
Ginsi Paulo alivyowaarifu wasomaji wake, wote walijua sheria, lakini hawawezi kuishika, wanahukumiwa, kwayo. (anagalia Warumi 7:22-24).Vile vile wale wote wanaomwamini Kristo hawaukumiwi, lakini wanaokolewa kwa kutijitoa kwake (angalia Warumi 8:3).

8:2 Kwa sababu sheria ya Roho wa uzima ule ulio katika Kristo Yesu imeniacha huru na sheria ya dhambi ni mauti.
Sheria: - Vitu fulani inayotiliwa na sherikali; sheria ya Musa (vile 8:3)
Roho: - Sehemu isiyoonekana ya mtu
Uzima: - Kinacho tafautisha kiumbe kinacho ishi na kya kukufa.
Huru: Kutokuwa chini ya ulinzi wa mtu au utawala fulani
Dhambi: - Kukiuka, kutotii sheria ya dini (vile vile 8:3)
Kifo:- Uharibifu wa kiroho au kimwili

“Roho wa uzima” hi Roho wa Yesu Kristo (Wafilipi 1:19), ambaye ni msingi wa “maisha” (Yohana 14:6). Kupitia kifo chake msalabani, waamini wamewekwa huru na Kristo, na haweesabiliwi tena kifo cha kiroho.

8:3 Maana yale yasiyowezekana kwa sheria, kwa vile ilivyokuwa dhaifu kwa sababu ya mwili, Mungu, kwa kumtuma Mwanawe menyewe katika mfano wa mwili ulio wa dhambi, alihukumu dhambi katika mwili.
Mwili: 4561 *sarx* – mwili wa kawaida

Sheria ya matendo mema au mabaya hayawezi kuokoa watu, lakini kuhukumu tabia mbaya tu.Kufanya wokovu uwezekane, Baba alimtuma Yesu katika umbo la mwanadamu ili akapate kusinda dhambi kupitia kifo chake na pale akaaribisha nguvu zake za kutuukumu.

9. Matumizi – Warumi 8:1-3
Kufurahiya katika maisha Mungu amenipatia kupitia imani yangu kwa Yesu na kuwa mwenye kushukuru ya kwamba kifo hakina tena uwezo juu yangu (Neno la msingi la kukumbuka ni maisha).
1O. Funga kwa Maombi

11. Kazi ya ziada – Hatua 7:
a.*Nidhamu 1: Mwabudu Bwana:* Tazamia Ukuu wa Mungu/Uzuri wake
b.*Nidhamu 2: Sikiliza Neno Lake:* Warumi 10-12/Tia akilini Warumi 10:9
c. *Nidhamu 3: Omba Mapenzi Yake:* Mwitikie Mungu unaposama Warumi 10-12
d.*Nidhamu 4: Ungana na Watu Wake:* Jiingize katika ushirika na kufanya wafuasi
e. *Nidhamu 5: Elezea dunia :* Changia *Ombi* na angalau watu 3
f. The Master Plan of Evangelism : Mlango wa 7- Soma na Tia alama
g. Jifunze Biblia : Kuwa na uzoefu na Greek Lexicon

HATUA YA 7

Hatua

Kristo



1. Fungua kwa Maombi

2. Rudilia *Ombi ya kujitoa* na *Safari* – Warumi 3:23, 6:23, 8:3, 10:9

3. Nidhamu za kiroho – Uliza Maswali yafuatayo:

a.*Nidhamu 1:* Ni ginsi gani wakati wako wa mwabudu umegusa maisha yako?

b. *Nidhamu 2:* Mungu alikunenea nini ulipokuwa nasoma Warumi 10-12?

c. *Nidhamu 3:* Mungu alikuongoza kuombea nini wakati ulikuwa na soma Andiko?

d.*Nidhamu 4:* Ulifanya ushirika na nani? Na iliendelea je ?

e. *Nidhamu 5:* Ulicyangiya injili na nani ?

4. The Master Plan of Evangelism– Ulivyochagua kutoka Mlango wa 7

5. **Vifaa vya Mafunzo ya Biblia –Tia katika matendo ukitumia Greek Lexicon**

6. Changia /Abudu/Omba:

a.*Changia* – Maswala binafsi ya kujukumika kwa ujasiri

b.*Abudu* – Tambua Ukuu wa Mungu /Shukuru Uzuri wa Mungu

c. *Omba* –Maswala ya kujukumika/Mtazamo katika Neno la Mungu: Warumi 10:8-10

7. Mtazamo –Warumi 10:8-10:

a. Soma Warumi 10:8-10 kutoka katika matafsiri mawili kwa *kuona mtazamo Kubwa.*

b. Acha wanafunzi watoe mtazamo katika maandiko ili wakapate *kuhisi mtazamo kubwa.*

Mfano:

Maandiko yanasema kwamba neno la imani hii karibu, na wale wanaomkiri Yesu kama Bwana na kuamini Mungu alimfufua katika wafu wataokolewa.

8. Utafsiri – Warumi 10:8-10

a. Ambia wanafunzi wasome kila mstari (mifano zilizo chini zimetoka katika BTK).

b. Ambia wanafunzi watoe maana ya Lexicon ya Maneno Msingi katika kila mstari.

c. Ambia wanafunzi watafsiri kila mstari kutumia akili zao & viombo vya mafunzo.

d. Jadili maana ya kila neno katika kila mstari katika context yake.

10:8 Lakini yanenaje? Lile neno li karibu nawe, katika kinywa chako, na katika moyo wako, yaani, ni lile neno la imani tulihubirilo.
Neno 4487 *rhema* - Yale yananayo semwa.
Moyo 2588 *kardia* - Moyo; kiti na katikati ya maisha ya mwanadamu,
Imani: 4102 *pistis* – Chamchemi ya kuamini
tulihubirilo 2784 *kerusso* – Kuubiri, kutoa ujumbe.

"Haki iliyo katika imani" (Warumi 10:6) sio sheria mpya ya dini ambayo Paulo anasema; lakini imekuwepo tangu wakati Mungu alipompatia Musa zile amri (Kumbukumbu la Torati 30:14).

10:9 Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na Kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka.

Kukiri: 3670 *homolegeo* – kuitika/kukubali (vile vile10:10)
Bwana: 2962 *kurios* – Bwana, mwenye mamlaka, jina la heshima
Amini: 4100 *pisteuo* – Kuamini, kuwa na msukumo wa imani (vile vile 10 :10)
Wafu : 3498 *nekros* – Kunyimwa uzima, kisicho kuwa hai tena
Kuokoka : 4982 *sozo* –Kuokoa, kutoa katika hatari, kutoa katika dhambi (vile vile 10 :10)

Paulo amekuwa akihubiri mafundisho ya haki kwa imani ambayo inaokoa wale wanao itambua wazi (Mathayo 10:32) ya kwamba Yesu ni Bwana Mkuu na wanaitika (Matendo 8:37) yakwamba Mungu alimfufua katika wafu.

10:10 Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu.

Kupata haki 1343 *dikaiosure* - Kufikia kiwango cha uhaki na usawa

Imani katika ufufuo wa Yesu na kukubali kwamba yeye ndiye mamlaka ya juu (Warumi 10:9) wanapaswa okolewa na kufanywa sawa na Mungu.

9. Kutia katika Matendo-Warumi 10:8-10
Kukiri Yesu kama Mwokozi na Bwana, kukiri kama imani ndani yake ndio njia pekee ya wokovu. (Neno msingi la kukumbuka ni kukiri).

10. Kazi ya ziada – Hatua 8:
a.*Nidhamu 1 : Mwabudu Bwana:* Tazamia Ukuu wa Mungu na Uzuri wake
b.*Nidhamu 2: Sikiliza Neno Lake :* Warumi 13-16/Tia akilini Warumi 13:10
c. *Nidhamu 3: Omba Mapenzi Yake:* Itikia Mungu unaposoma Warumi 13-16
d. *Nidhamu 4: Ungana na Watu Wake:* Ungana katika Ushirika na Ufuasi
e.*Nidhamu 5: Elezea Dunia:* Changia *Ombi* na angalau watu 3
f. The Master Plan Evangelism : Mlango wa 8- Soma na utie alama
g. Jifunze Biblia : Kuwa na uzoefu na vifaa vinavyo patikana.

HATUA YA 8

Kusudi

Kristo



1. Fungua kwa Maombi

2. Rudilia *Ombi* na *Safari* – Warumi 3:23, 6:23, 8:3, 10:9, 13:10

3. Nidhamu za kiroho – Uliza maswali yafuatayo:

a. *Nidhamu 1:* Ni ginsi gani wakati wako wa maabudu umebadilisha maisha yako?

b.*Nidhamu 2:* Mungu alinena nini nawe wakati ulipokuwa unasoma Warumi 13-16?

c.*Nidhamu 3:* Mungu alikuongoza kuombea nini wakati ulikuwa na soma Andiko?

d. *Nidhamu 4:* Ulifanya ushirika na nani? Na iliendelea je ?

e.*Nidhamu 5:* Ulicyangiya injili na nani, iliendelea vipi ?

4. The Master Plan of Evangelism – Ulivyochagua kutoka Mlango wa 8

5. **Vifaa vya Mafunzo ya Biblia –Jifunze kupitia Mtandao**

6. Changia /Abudu/Omba:

a. *Changia* - Maswala Binafsi katika ujasiri

b.*Abudu* – Tambua Ukuu wa Mungu /Shukuru Uzuri wa Mungu

c. *Omba* – Maswala ya kujukumika/Mtazamo katika Neno la Mungu (Warumi 13:8-10)

7. Mtazamo –Warumi 13:8-10:

a. Soma Warumi 13:8-10 katika matafsiri mawili ukapate *kuona mtazamo kubwa.*

b. Acha wanafunzi watoe mtazamo wakapate *kuhisi mtazamo kubwa.*

Mfano:

Wakristo awapaswi kuwa na deni ya wengine isipokuwa upendo kwa sababu upendo unatimiza sheria, ambayo inasomekana hivi “Penda jirani yako kama unavyo jipenda wewe.”

8. Utafsiri – Warumi 13:8-10

a. Acha wanafunzi wasome kila mstari (mifano pale chini zimetoka katika BTK).

b. Acha wanafunzi watoe maana ya Lexicon ya Maneno Msingi katika kila mstari.

c. Acha wanafunzi watafsiri kila mstari kutumikisha akili zao & vifaa vya mafundisho.

d. Tia mjadala juu ya kujadili maana ya maneno katika kila mstari katika context yake.

13:8 Msiwiwe na mtu cho chote, isipokuwa kupendana, kwa maana ampendae mwenzake ameishinda sheria.

Msiwiwe 3784 *opheilo* - Shurukizwa kufanya jambo fulani
Upendo 25 *agapao* - Kupenda kwa moyo sio kwa hisia (vile vile13:8-9)
Sheria 3551 *nomos* – Sheria ya Musa au sheria za serikali (vile vile13:10)

Paulo ananena hapa kuusu sheria ya Mungu, ambayo ni kujali wengine ambao ni tendo la hiyari. Kufanya hivi ni kutimiza sheria ya Mungu, ambao ni upendo ginsi Yesu alivyosema katika Matayo 22:36-40.

13:9 Maana kule kusema usizini, usiue, usiibe, usitamani, na ikiwapo amri nyingine yo yote, inajumlishwa katika neno hili, ya kwamba, mpende jirani yako kama nafsi yako.

Kuzini: 3431*moicheia* – Kufanya tendo ya ndoa kinyume cha sheria na mwanamke wa bwana mwingine
Kuua: 5407*phoneuo* – Kuua, kuua bila haki
Kuiba: 2813 *klepto* – Kuchukua cha mwingine bila ruhusa
Tamani: 1937*epithumeo* – Kuwa na tama juu ya kitu fulani
Jirani: 4139 *plesion* – aliye karibu nawe; jirani (vile vile13:10)

Paulo anaunga mkono maneno haya yalio katika 13:8 kwa kutia alama amri ya 6, 7,8 na ya 10 (angalia Kutoka 20:13-15, 17). Mtume anazitia maneno haya yote katika neno moja/amri moja (Walawi 19:18), ambayo inasema penda watu wote ginsi unavyojipenda mwenyewe.

13:10 Pendo halimfanyi jirani neno baya; basi pendo ndilo utilifu wa sheria.

Baya: 2556 *kakos* – matendo yasio sawa au mema

Paulo anasisitiza aliyoyasema katika 13:8-9, lakini ana geuza sheria, na kwa kufanya hivyo anaadhirisha kwa kusema upendo ni utimilifu wa sheria.

9. Matumizi -Warumi 13:8-10

Kutokuwa na kitu na mtu isipokuwa upendo, na kuonyesha kujitoa kwangu inafika mwisho kwa kumpenda jirani kama nafsi yangu (neno la msingi la kukumbuka ni upendo.)

10. Funga kwa Maombi

11. Kazi ya ziada ya siku za usoni/Mbele:

a. *Nidhamu 1: Mwabudu Bwana:* Endelea kumwabudu Bwana kila siku
b. *Nidhamu 2: Sikiliza Neno Lake:* Endelea kusoma Neno la Mungu na kutafakari
c. *Nidhamu 3: Omba Mapenzi Yake:* Endelea kuomba Mapenzi Yake kama inavyo funuliwa katika Neno Lake.
d. *Nidhamu 4: Ungana na Watu Wake*: Endelea kuungana na waamini na kufanya wafuasi
e. *Nidhamu 5: Elezea Dunia:* Endelea kuchangia *Ombi* na *Safari*.